Ghorofa ya Saba, LAPF Pensions Fund Tower; Mkabala na Kijiji cah Makumbusho, Kijitonyama; S.L.P 72175, DAR ES SALAAM; Simu: +255-22-2923513/8; Nukushi:+255-22-2923519
Barua Pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz

# TANGAZO KWA UMMA

## MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA KOROGWE ("KOROGWE WSSA") KWA MWAKA 2016/17 – 2018/19

**Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-16-012**

Mnamo tarehe 31Mei 2016 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Korogwe (KOROGWE WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2016/17 hadi 2018/19. Jedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

**Jedwali 1: Bei za Maji kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)**

| Aina za Wateja | Matumizi | Bei za Sasa | % Ongezeko | Bei Zilizopendekezwa (TZS/$m^3$) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 2016/17 | % Ongezeko | 2017/18 | % Ongezeko | 2018/19 |
| Majumbani | 0-7 | 440 | 166% | 1,170 | 10% | 1,287 | 10% | 1,416 |
| | >7 | 490 | 166% | 1,303 | 10% | 1,433 | 10% | 1,577 |
| Taasisi | 0-14 | 440 | 166% | 1,170 | 10% | 1,287 | 10% | 1,416 |
| | >14 | 500 | 166% | 1,330 | 10% | 1,463 | 10% | 1,609 |
| Biashara | 0-14 | 440 | 166% | 1,170 | 10% | 1,287 | 10% | 1,416 |
| | >14 | 500 | 166% | 1,330 | 10% | 1,463 | 10% | 1,609 |
| Viwandani | | 1000 | 166% | 2,660 | 10% | 2,926 | 10% | 3,219 |
| Magati | | 1000 | 166% | 2,660 | 10% | 2,926 | 10% | 3,219 |
| Matanki | | 1000 | 166% | 2,660 | 10% | 2,926 | 10% | 3,219 |

**Jedwali 2: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa(Shilingi/Mwezi)**

| Aina ya Wateja | Gharama za Sasa | % Ongezeko | Gharama Zilizopendekezwa 2016/17 – 2018/19 |
|---|---|---|---|
| Wateja Wote | - | | 2,000 |

**Jedwali 3: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Maunganisho ya Maji (Shilingi/Maunganisho)**

| Aina ya Wateja | Ada za Sasa | % Ongezeko | Ada Zinazopendekezwa 2016/17 – 2018/19 |
|---|---|---|---|
| Majumbani | 15,000 | 67% | 25,000 |
| Taasisi | 15,000 | 67% | 25,000 |
| Biashara | 15,000 | 67% | 25,000 |
| Viwandani | 15,000 | 234% | 50,000 |
| Magati | 15,000 | 67% | 25,000 |

**Jedwali 4: Ada ya Sasa na Inayopendekezwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)**

| Aina ya Wateja | Ada ya Sasa | % Ongezeko | Ada Zinazopendekezwa 2016/17 – 2018/19 |
|---|---|---|---|
| Majumbani | 5,500 | 82% | 10,000 |
| Taasisi | 5,500 | 82% | 10,000 |
| Biashara | 5,500 | 82% | 10,000 |
| Viwandani | 5,500 | 809% | 50,000 |
| Magati | 5,500 | 173% | 15,000 |

**Jedwali 5: Kodi ya Sasa na Inayopendekezwa ya Dira (Shilingi/Dira)**

| Aina ya Wateja | Kodi za Sasa 2015/16 | % Ongezeko | Kodi inayopendekezwa 2016/17 | % Ongezeko | Kodi inayopendekezwa 2017/18 – 2018/19 |
|---|---|---|---|---|---|
| Majumbani | 1,500 | 33% | 2,000 | 25% | 2,500 |
| Taasisi | 2,000 | 25% | 2,500 | 20% | 3,000 |
| Biashara | 2,000 | 25% | 2,500 | 20% | 3,000 |
| Viwandani | 10,000 | 20% | 12,000 | 25% | 15,000 |

KOROGWE WSSA imeeleza kuwa, bei zinazopendekezwa zitaisaidia kumudu gharama za uendeshaji angalau kwa asilimi 90, kuhimili mabadiliko ya viashiria vya kiuchumi na gharama ndogo za uwekezaji. KOROGWE WSSA pia, imeeleza faida zitakazopatikana ikiwa ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma za maji.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Ijumaa, tarehe 26 Agosti 2016 katika Ukumbi wa Halmashauri ya mji wa Korogwe** kuanzia **saa nne kamili (4.00) asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu ndani ya kipindi cha siku 14 baada ya Mkutano (**Ifikapo tarehe 10 Septemba 2016**). Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi ya EWURA, **GHOROFA YA SABA, LAPF PENSIONS FUND TOWER; MKABALA NA KIJIJI CHA MAKUMBUSHO, KIJITONYAMA, DAR ES SALAAM** au **ofisi za KOROGWE WSSA, KOROGWE**.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamalaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**
**5 Agosti 2016**